JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

AHADI YA UADILIFU KWA VIONGOZI WA UMMA, WATUMISHI WA UMMA NA SEKTA BINAFSI

S. L. P. 13341,
DAR ES SALAAM.
Simu: 2111810/1
Barua Pepe: secretariat@ethics.go.tz
Tovuti: www.ethicssecretariat.go.tz

AHADI YA UADILIFU KWA VIONGOZI WA UMMA, WATUMISHI WA UMMA NA SEKTA BINAFSI TANZANIA

1.0 MAANA YA AHADI YA UADILIFU

Ahadi ya Uadilifu ni tamko rasmi na bayana la dhamira ya kuwa mwadilifu na kuunga mkono Kampeni ya Kitaifa ya Maadili na Mapambano dhidi ya Rushwa.

Ni Hati ambayo inatoa fursa kwa Kampuni au Afisa wa Umma kutoa ahadi ya kuzingatia Kanuni za Maadili na Mkakati wa Mpambano dhidi ya Rushwa katika Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Tanzania. Kwa kuweka sahihi Hati ya Ahadi ya Uadilifu; Kampuni, Kiongozi au Mtumishi wa Umma anakuwa amekubaliana na masharti kuwa:

i) atazingatia misingi ya uadilifu, uwajibikaji, uwazi na weledi katika kufanya biashara au kutekeleza majukumu ya umma;

ii) atazingatia masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma na Kanuni za Maadili ya Kitaaluma;

iii) atakuwa mzalendo kwa nchi yake na mtii kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

iv) atalinda mazingira na mali ya umma.

2.0 CHIMBUKO LA WAZO LA KUWA NA AHADI YA UADILIFU

Wazo la kuwa na Ahadi ya Uadilifu liliibuliwa katika maabara ya Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN). Ilionekana kuwa pamoja na kuwepo Sheria, Kanuni, Miongozo na Mikakati ya Kukuza Maadili na Kupambana na Rushwa, bado rushwa ipo na lazima iendelee kupigwa vita. Wananchi wameendelea kusumbuliwa na urasimu usio wa lazima na utoaji huduma usioridhisha unaotengeneza mazingira ya rushwa.

Aidha, huko nyuma Sekta Binafsi haikushirikishwa vya kutosha katika Mkakati wa Mapambano dhidi ya Rushwa. Rushwa inaonekana ni tatizo la Sekta ya Umma wakati ambapo wanaotoa na kupokea rushwa wako pia katika Sekta Binafsi.

Ni dhahiri kuwa Sheria, Kanuni, Miongozo na Mikakati iliyopo haiwezi peke yake kupunguza au kumaliza kabisa tatizo la rushwa na utovu wa maadili. Lazima Wadau wote washirikishwe katika mkakati wa kukuza na kusimamia maadili nchini. Ahadi ya Uadilifu ni fursa muhimu kwa Sekta Binafsi, Viongozi na Watumishi wa Umma kuonesha utayari wao kushiriki mapambano dhidi ya rushwa na utovu wa maadili.

3.0 UMUHIMU WA AHADI YA UADILIFU

Ahadi ya Uadilifu ina umuhimu ufuatao:

i) Inaimarisha mapambano ya kisheria dhidi ya rushwa na makosa mengine ya kiuadilifu;

ii) Inachochea utashi wa wale waliosaini Hati hizo kuishi na kuenenda katika misingi ya uadilifu;

iii) Inatoa fursa ya kujipima na kujitathimini wenyewe tofauti na mifumo ya kisheria ambayo msisitizo wake ni kutoa adhabu mara baada ya kitendo kutokea;

iv) Inachochea hali ya nadhiri ya mtu kumsuta na hivyo kumfanya atii bila shuruti; na

v) Inasaidia kujenga utamaduni wa kuheshimu maadili badala ya watu kushinikizwa kuyafuata maadili bila kuyaamini maadili yenyewe.

4.0 MISINGI YA AHADI YA UADILIFU

Hati ya Ahadi ya Uadilifu imetilia maanani misingi ifuatayo ya maadili na mapambano dhidi ya rushwa:

i) Kukuza Uwazi, Uadilifu, Uwajibikaji na Utaalamu katika uendeshaji shughuli za umma;

ii) Kukuza mwitikio wa kupambana na rushwa kwa kuimarisha taratibu za udhibiti wa ndani;

iii) Kusimamia masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma, na Kanuni za Maadili ya Kitaaluma;

iv) Kuimarisha mahusiano ya Viongozi wa Umma, Watumishi wa Umma au wamiliki na Watendaji wa Makampuni na wananchi au wateja wengine;

v) Kudhibiti vitendo vya utovu wa maadili mahali pa kazi;

vi) Kukuza uzalendo, utii kwa Serikali, ulinzi wa mazingira na mali ya umma;

vii) Kuainisha bayana matarajio ya wananchi kwa Makampuni, Viongozi wa Umma na Watumishi wa Umma.

Kwa ujumla Hati ya Ahadi ya Uadilifu imezingatia misingi ya Uadilifu (Integrity), Uwajibikaji (Accountability) na Weledi (Professionalism).

5.0 MAMLAKA YA KUTAYARISHA NA KUSIMAMIA UTEKELEZAJI WA AHADI YA UADILIFU

Kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya 1995, Mhe. Rais ana wajibu wa kushughulikia ukuzaji wa uadilifu katika Ofisi za Umma na kuishirikisha Sekta Binafsi katika mkakati huo. Lengo ni kuweka msingi wa kuongeza imani ya wananchi kuhusu uadilifu wa Viongozi wa Umma katika kufanya maamuzi ya Serikali.

Jukumu la kuratibu utayarishaji na kusimamia utekelezaji wa Ahadi ya Uadilifu kwa Viongozi wa Umma, Watumishi wa Umma na Makampuni katika Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) liko chini ya Sekretarieti ya Maadili

ya Viongozi wa Umma ambayo ni chombo kikuu cha kukuza na kusimamia maadili ya uongozi nchini.

Pia kwa mujibu wa Kanuni ya 66 (2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, kila mtumishi wa umma anatatakiwa kusaini tamko la kuzingatia Kanuni za Maadili ya Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma. Kanuni hizo zimezingatiwa ipasavyo katika Ahadi ya Uadilifu. Mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa tamko hilo yako chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Mamlaka za Nidhamu za Watumishi wa Umma.

Aidha, Makampuni yanawajibika kujisajili na kupata Leseni za biashara chini ya Sheria ya Makampuni Sura ya 212 kutoka kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ambaye anawajibu wa kuhakikisha Makampuni yanaendesha shughuli zake kwa kuzingatia misingi ya uendeshaji bora wa biashara.

6.0 UTOAJI WA HATI YA AHADI YA UADILIFU

6.1 Wajibu wa Wasimamizi wa Ahadi ya Uadilifu

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) zitakuwa na wajibu wa kutoa Hati ya Ahadi ya Uadilifu kwa Viongozi wa Umma, Watumishi wa Umma na Makampuni binafsi kila mmoja kulingana na mamlaka iliyonayo;

Taasisi Simamizi, Wizara, Idara za Serikali Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, Makampuni binafsi na wananchi watakuwa na wajibu wa kusimamia utekelezaji wa Ahadi ya Uadilifu;

Sekretarieti ya Maadili na Mamlaka zilizotajwa zina wajibu wa kuandaa orodha ya wanaotakiwa kusaini Hati ya Ahadi ya Uadilifu; [1]

BRELA ina wajibu wa kuhakikisha kuwa Makampuni yanafuata utaratibu wa kushughulikia nyaraka za kampuni kwa kugonga muhuri Hati ya Ahadi ya Uadilifu baada ya kusainiwa na Mtendaji Mkuu wa Kampuni husika;

[1] Hati hizo ni kama zinavyoonekana katika Kiambatanisho “A”

Kamishna wa Maadili, Mtendaji Mkuu wa Wizara, Idara za Serikali Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na Mtendaji Mkuu wa BRELA watasaini Hati hizo kama wasimamizi wa utekelezaji kila mmoja kwa mamlaka aliyonayo;

Mamlaka zilizotajwa zitawajibika pia kushiriki katika Kampeni ya Kitaifa ya Maadili na kutoa elimu kuhusu maudhui na umuhimu wa Ahadi ya Uadilifu katika mapambano dhidi ya rushwa na utovu wa maadili.

Mamlaka za ajira zina wajibu wa kuhakikisha kuwa Ahadi ya Uadilifu inakuwa sehemu ya barua ya ajira na uteuzi wa Viongozi na Watumishi wa Umma kama zilivyoambatanishwa na maelezo haya.

7.0 KUSAINI HATI YA AHADI YA UADILIFU

7.1 Wajibu wa Wanaotakiwa Kusaini Ahadi ya Uadilifu

Viongozi wa Umma wote waliotajwa katika Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Watumishi wote wa Umma katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makampuni binafsi yanayoendesha shughuli zake ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yatawajibika kusaini Hati ya Ahadi ya Uadilifu na kuwasilisha kwa mamlaka inayohusika.

Watumishi wanaofanya kazi katika Utumishi wa Umma kwa masharti ya Mkataba wanalazimika kusaini Hati ya Ahadi ya Uadilifu kama ilivyo kwa Watumishi wengine wa Umma;

Baada ya kusaini Hati hiyo wanawajibika kutekeleza masharti yote yaliyoko katika Hati ya Ahadi ya Uadilifu;

Pia, wanawajibika kushirikiana na Taasisi simamizi kuhakikisha kuwa kila aliyesaini anatekeleza masharti ya Ahadi ya Uadilifu;

Aidha, wana wajibu wa kushiriki katika Kampeni ya Kitaifa ya Maadili na elimu kuhusu maudhui na umuhimu wa Ahadi ya Uadilifu katika mapambano dhidi ya rushwa na utovu wa maadili.

8.0 MUDA WA KUSAINI HATI YA AHADI YA UADILIFU

Muda wa kusaini utakuwa:

i) Mara moja tu kwa kampuni ambayo Mtendaji wake Mkuu aliyesaini bado yuko madarakani;

ii) Zaidi ya mara moja kwa Makampuni ambayo Watendaji Wakuu wake wamebadilika, hivyo zitalazimika kusaini upya Hati ya Ahadi ya Uadilifu wakati wa kuhuisha nyaraka BRELA.

iii) Mara moja tu kwa Viongozi wa Umma au Watumishi wa Umma ambao wako katika nyadhifa ambazo walikuwa nazo wakati wakisaini Hati ya Ahadi ya Uadilifu;

iv) Zaidi ya mara moja kwa Viongozi wa Umma na Watumishi wa Umma waliopanda vyeo au kuteuliwa katika nyadhifa mpya, hivyo watalazimika kusaini Hati nyingine ya Ahadi ya Uadilifu;

v) Aidha, Viongozi wa Umma na Watumishi wa Umma wapya wanatarajiwa kusaini Ahadi ya Uadilifu mara tu wanapoteuliwa, wanapochaguliwa au wanapoajiriwa;

vi) Mtumishi anapohama Wizara, Idara ya Serikali Inayojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi ya Umma, Shirika la Umma au Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwenda Ofisi nyingine ya Umma atalazimika kusaini Hati nyingine ya Ahadi ya Uadilifu;

Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Namba 2 wa mwaka 2015 kuhusu Utekelezaji wa Ahadi ya Uadilifu umetolewa na kuanza kutumika mwezi Agosti, 2015.

9.0 ATHARI ZA KUKIUKA MASHARTI YA AHADI YA UADILIFU

Ukiukaji wa masharti ya Ahadi ya Uadilifu unaweza kusababisha:

i) Kupoteza imani kwa wananchi na makampuni washirika wa kibiashara;

ii) Kupoteza vigezo vya kufanya biashara na Serikali;

iii) Kuchukuliwa hatua za kinidhamu au kisheria kwa uvunjaji wa masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sheria ya Ununuzi wa Umma,

Sheria za Utumishi wa Umma, Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma na miongozo inayotolewa na Serikali.

10.0 MCHAKATO WA KUANDAA NA UTEKELEZAJI WA AHADI YA UADILIFU

Mchakato wa kuandaa na utekelezaji wa Ahadi ya Uadilifu unahusisha hatua zifuatazo:

i) Kuandaa rasimu ya Ahadi ya Uadilifu;

ii) Kukutana na wadau wa ndani na nje kwa ajili ya kupata maoni;

iii) Kuchambua maoni ya wadau na kuandaa Rasimu ya mwisho;

iv) Rasimu kuidhinishwa na kutolewa waraka wa utekelezaji wake;

v) Ahadi ya Uadilifu kusambazwa na kusainiwa na Makampuni, Viongozi na Watumishi wa Umma;

vi) Ufuatiliaji na Tathmini;

vii) Utafiti kubaini hali ya uzingatiaji wa maadili kwa Viongozi, Watumishi wa Umma na Sekta Binafsi.

11.0 HITIMISHO

Inategemewa kuwa utekelezaji wa Ahadi ya Uadilifu utajenga mwitikio na dhamira ya uadilifu, uwazi, uwajibikaji, ari ya kupambana na rushwa na utoaji wa huduma bora katika Sekta ya Umma na Binafsi.

Pia, utahamasisha Viongozi, Watumishi wa Umma na Sekta Binafsi kuzingatia misingi ya maadili na mapambano dhidi ya rushwa. Aidha, kuwashirikisha wananchi kufuatilia vitendo vya utovu wa maadili miongoni mwa Watumishi wa Umma, Viongozi wa Umma na Sekta Binafsi na kutoa taarifa kwa mamlaka husika.